

Kudhibiti Matumizi Yako ya Pesa

Daftari hili litakusaidia . . .

- ▶ kuelewa tofauti kati ya **vitu unavyohitaji** na **vitu unavyotaka**.
- ▶ kuamua ama **kutumia pesa** au **kuzihifadhi**.
- ▶ kuamua ikiwa utanunua kitu **sasa** au **baadaye**.



TOFAUTI KATI YA VITU UNAVYOHITAJI NA VITU UNAVYOTAKA

Hatari: **KUTOELEWA TOFAUTI.**

Hakuna ubaya wa kununua vitu *unavyotaka*. Jambo kuu ni kufahamu vitu vya kutanguliza. Biblia inasema hivi: “Mhakikishe mambo muhimu zaidi.”—Wafilipi 1:10

Andika baadhi ya vitu unavyohitaji na vitu unavyotaka kwa muda wa mwezi mmoja. Katika orodha hiyo, andika vitu ambavyo wewe unatazamiwa kuvilipia.

Jambo la kufikiria: Kitabu *The Complete Guide to Personal Finance: For Teenagers and College Students* kinasema hivi: “Wakati mwingine si rahisi kutofautisha kati ya vitu tunavyohitaji na vitu tunavyotaka, . . . vitu vingi ambavyo unafikiri unavihitaji mara nyingi ni vile ambavyo unavitaka, na baada ya muda hutavihitaji tena.”

Ukiwa na wazo hilo akilini, je, kuna kitu chochote unachotaka ambacho umekiorodhesha chini ya “vitu unavyohitaji”?

Mwezi

.....

VITU UNAVYOHITAJI

(vitu vya lazima ambavyo utalipia kwa pesa zako—si vile ambavyo wazazi wako wanakunulia)

VITU UNAVYOTAKA

(vitu ambavyo si mahitaji ya msingi kama vile burudani, tafrija, na vitu *unavyopenda* kununua)

TOFAUTI KATI YA KUTUMIA PESA NA KUZIHIFADHI

Hatari: **KUTUMIA PESA KUPITA KIASI.**



“Si ushamba kununua vitu vizuri vinavyouzwa kwa bei nafuu na kuhifadhi pesa kidogo-kidogo. Unapofanya hivyo utakuwa na pesa zaidi kwa ajili ya vitu unavyohitaji na vitu unavyotaka.”—*I’m Broke! The Money Handbook.*

“Hata ikiwa bei ya kitu imepunguzwa, ninaweza kuhifadhi pesa zangu zote ikiwa sitanunua kitu hicho!”—Danielle

Orodhesha baadhi ya vitu ambavyo uliwahi kununua halafu baadaye ukajuta kwa sababu ulihitaji pesa kwa ajili ya kitu kingine.

Kitu

Gharama

_____	_____
_____	_____
_____	_____
_____	_____

Jumla ya gharama ya kununua vitu hivyo



Kadiri ni kiasi gani unachoweza kuhifadhi kwa mwezi mzima ikiwa hutanunua vitu usivyohitaji au kufanya mambo yanayokupotezea pesa.



Zidisha gharama hizo mara 12 ili uone ni pesa ngapi ambazo ungeweza kuhifadhi kwa mwaka mzima.

x12

=

Jambo la kufikiria: Biblia inasema kwamba “anayependa raha atakuwa maskini.” (Methali 21:17) Mtazamo wako kuelekea burudani na starehe unaathirije matumizi yako ya pesa?

TOFAUTI KATI YA HALI ZA SASA NA ZA BAADAYE

Hatari: **KUNUNUA VITU BILA KUPANGA.**

“Ikiwa ninatamani kununua kitu fulani, ninajaribu kusubiri kwa majuma kadhaa ili kuhakikisha kama kweli bado ninahitaji kitu hicho na kwamba nitaweza kukitumia vizuri.”—Alana



Ni wakati gani hasa wewe hununua vitu bila kupanga?

- Unapoviona kwenye Intaneti
- Ukiwa matembezi na marafiki
- Unapojisikia vibaya
- Mara tu ninapopokea mshahara au ninapopata pesa

Orodhesha baadhi ya faida za kusubiri kabla ya kufanya ununuzi mkubwa.

Jambo la kufikiria: Unaweza kujiwekea malengo gani ili kudhibiti matumizi yako ya pesa?

BAJETI YANGU YA MWEZI

Bajeti inaweza kukusaidia kudhibiti matumizi ya pesa zako.

Katika safu ya kwanza, orodhesha pesa unazotarajia kupata kwa mwezi mzima. Katika safu ya pili, orodhesha jinsi utavyotumia pesa hizo. Na kadiri siku zinavyosonga katika mwezi, andika pesa halisi unazotumia kwa ajili ya kila kitu ulichoandika.

Kipato

KUTOKA KWA WAZAZI

KUTOKANA NA KAZI YA MUDA

KUTOKA SEHEMU NYINGINE

Jumla

Bajeti ya Matumizi



CHAKULA

.....



NGUO

.....



SIMU

.....



BURUDANI

.....



MCHANGO

.....



AKIBA

.....



GHARAMA ZA NYUMBANI

.....

Jumla

Kiasi Halisi Nilichotumia

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Jumla